

# Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapojivunia siku 100 ya Rais Samia Suluhu Hassan

Na Moshi Lusonzo

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imejizatiti kutekeleza mikakati ya kuhakikisha serikali na wananchi wananufaika moja kwa moja na uzalishaji wa mazao na bidhaa inayotokana na sekta hizo.

Mkakati huo umewekewa mkazo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuingia madarakani na matunda yake yameanza kuonekana ikiwamo kuongezeka kwa mapato yatokanayo ya shughuli ya ufugaji na uvuvi wa bahari na kwenye maziwa makuu.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema kazi hizo ni zile zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021, na kuwekewa mkazo ndani ya siku 100 ya serikali ya awamu ya sita.

Waziri Ndaki, anasema baadhi ya kazi hizo zimetokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa katika matukio mbalimbali ili kuboresha sekta za mifugo na uvuvi.

## UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

Katika kipindi cha siku 100 ya Serikali ya awamu ya Sita, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mifugo ni mengi, lakini kwa kiasi kikubwa ni kuendeleza miundombinu ya ufugaji na kuboresha masoko.

Waziri huyo anasema katika kipindi hicho, Wizara imechimba visima virefu viwili katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa eneo la Usolanga na Mpapa Halmashauri ya Manyoni.

Pia, anasema wamekarabati mabwawa matatu ya Chamakweza halmashauri ya Chalinze, Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro), na kazi imekamilika kwa asilimia 100.

"Tumetenga hekta 32,044.21 katika Wilaya za Tanganyika, Nsimbo na Mlele kwa ajili ya malisho ili kuongeza thamani mifugo yetu," anasema Waziri Ndaki.

Ili kuboresha bidhaa ya mifugo, wizara hiyo imetoa mafunzo na kutoa leseni kwa wachunaji ngozi 340 wa machinjio za Manispaa ya Kinondoni na Temeke jijini Dar es Salaam.

"Pamoja na mafunzo hayo, tumewapatia vitendea kazi wakaguzi wa Ngozi 34 wa Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara. Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani na nje ya nchi," amezidi kueleza.

Katika kuongeza kasi ya biashara na kuwapatia wafugaji kipato, serikali imefungua mnada wa mifugo wa mpakani wa Magena, mkoani Mara ili kuwezesha biashara ya mifugo kati ya Tanzania na Kenya kuendelea. Pia, ujenzi wa mnada wa mifugo wa upili wa Buzirayombo, mkoani Geita umefikia asilimia 50.

Aidha, jumla ya ng'ombe wa asili 197 katika mikoa ya Iringa walifanyiwa uchambuzi ili kubaini na kutunza mbari za asili.

## USHIRIKIANO NA ZANZIBAR

Waziri Ndaki, anasema katika kipindi hicho Wizara ya Mifugo na Uvuvi upande wa mifugo, na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zimefanya kikao na kukubaliana kuendeleza ushirikiano kiutendaji katika ngazi za idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo ni kuimarisha sekta za mifugo katika pande zote mbili za muungano ili ziweze kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi.

## SEKTA YA UVUVI

Sekta ya Uvuvi ni moja kati maeneo yanayokuwa kiuchumi kwa haraka hapa nchini. Shughuli za uvuvi huchangia katika kuwapatia wananchi uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato na kupunguza umaskini.

Kutokana na umuhimu wake, serikali imekamilisha ujenzi wa majengo matatu ya ofisi kwa ajili ya vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMU) katika Wilaya za Pangani katika kijiji cha Kipumbwi, Mkinga kijiji cha Zingibari na Bagamoyo kijiji cha Dunda.

Katika maeneo ya maziwa, wizara imeboresha miundombinu wezeshi uvuvi kwa kuanza ujenzi wa mialo sita katika kanda ya ziwa Victoria, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay-Nyasa Mkoani Ruvuma, na kutangazwa kwa zabuni ya kupata Mkandarasi wa Ukarabati wa Soko la Samaki la Feri, jijini Dar es Salaam utakaoanza mwezi Julai, mwaka huu.

Pia, imetengwa Sh. bilioni 50 katika bajeti ya 2021/2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Mbegani Wilaya ya Bagamoyo.

"Kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari Kuu zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 tarehe 23 Aprili, mwaka huu, yote haya ni kwajili ya manufaa ya wananchi ", amezidi kusisitiza Waziri Ndaki.

## FURSA ZA UWEKEZEJI

Serikali imetangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya uvuvi kupitia mikutano mbalimbali ya kitaifa iliyojumuisha wageni kutoka nje.

Nchi zilizoshiriki ni Ufalme wa Saudi Arabia, China na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Mikutano hiyo ilipelekea kwa mara ya kwanza Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kukusanya jumla ya dola za Marekani 800, 000 sawa na Sh. bilioni 1.84 kama malipo ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu kwa meli 22.

Mafanikio hayo yamepatikana baada ya meli za kigeni kusitisha kuchukua leseni za Tanzania kuanzia mwaka 2017 kulikosababisha serikali kukosa mapato na DSFA kushindwa kujiendesha.

"Katika kuhakikisha hakuna meli inayosumbuliwa, tumenunua boti 12 na injini sita za kupachika kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi," anaongeza kusema.

Aidha, DSFA ilikamilisha maandalizi na kuwezesha mawaziri wenye dhamana ya Sekta ya Uvuvi pande mbli za muungano kusaini kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2021 na kuanza kutumika rasmi Aprili 23, mwaka huu.

Ili kunufaika na fursa za Uchumi wa Buluu kupitia tasnia ya ukuzaji viumbe maji, Serikali imetenga Sh. bilioni 18 ambazo zitatumika kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu katika vituo sita vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Mwamapuli mkoani Tabora, Ruhila (Ruvuma), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi), Machui (Tanga), na Rubambagwe mkoani Geita.

Katika mkakati huo mashamba darasa 40 ya ufugaji samaki yatayosimamiwa na vikundi vya vijana na kinamama. Huu ni mwanzo wa utelekezaji wa azma ya kuwa shamba darasa katika kila halmashauri nchini ili kuhamasisha ufugaji wa samaki nchini kwa ajili kuboresha lishe, kuongeza kipato na kukuza uchumi wa wananchi wa kawaida.

Aidha, ili kuhamasisha umefanyika wa ukuzaji viumbe maji bahari, wakulima wa mwani katika maeneo ya Mkinga mkoani Tanga na Mchinga mkoa wa Lindi. Pia wafugaji wa majongoo bahari wilaya ya Bagamoyo wamenunuliwa vitendea kazi vyenye thamani ya shilingi 15,000,000.00 ili waweze kuongeza uzalishaji.

Scanned with CamScanner

# Makala akerwa mazingira mnada wa ng'ombe Pugu

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ameelezea kutoridhishwa na miundombinu ya mnada wa ng'ombe Pugu na kumwagiza mkandarasi kufanya marekebisho.

Alitoa maagizo hayo jana alipofanya ziara ya kushtukiza katika mnada huo baada ya kupata taarifa za malalamiko ya wananchi kuitaka serikali iingilie kati uboreshaji wa eneo hilo.

Pia Makala alionyesha kutoridhishwa na tabia ya watendaji kutengeneza urasimu na kuchelewesha uboreshaji wa mnada huo ikiwamo ujenzi wa uzio, sakafu, eneo salama la kupakilia ng'ombe, vyoo na kero ya ukosefu wa maji.

"Mazingira niliyoyaona eneo hili na huo urasimu uliopo hautoi matumaini. Kama mtaendelea na mambo yenu ya tathmini, njooni 'site' (eneo la kazi), kazi zinazotakiwa kufanywa zifanywe, za kufanyia tathmini ziendelee lakini kazi iendelee muwapo eneo la kazi.

"Hivi ni vitu vidogo wakati mnaendelea na tathmini ya kujenga ukuta anzeni kurekebisha na vitu vingine. Ng'ombe hapa usalama wake haupo, yaani jinsi palivyo ni sawa na mnada wowote wa kijijini. Sijaridhishwa hata kidogo, naomba lifanyiwe kazi," alisema Makala.

Aliongeza kuwa mambo madogo ya urasimu yanayofanywa na watendaji hao ndiyo yanayojenga imani mbaya kwa wananchi kuwa viongozi wa serikali hawaendi na kasi inayotakiwa katika kushuhulika na kero za wananchi.

Pia aliagiza kuondolewa mara moja matofali yaliyokusanywa katika eneo hilo kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wa ukuta unaozunguka mnada huo baada ya kubaini kuwa hayana ubora.

Scanned with CamScanner

Mwananchi Uk.10, Julai 10,2021

# Mradi wa machinjio Vingunguti ukamilike

Moja ya habari kubwa zilizoripotiwa na gazeti hili jana ni agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala kwa uongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) la kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa machinjio ya Vingunguti unakamilika.

Makala alitoa agizo hilo alipotembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huo uliotakiwa kukamilika tangu Desemba 2019.

Huu ni mlolongo wa amri mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa na viongozi kila wanapotembelea mradi huo ulioanza kutekelezwa Juni 2019.

Orodha ya viongozi hao ni ndefu; lakini itoshe tu kusema wapo viongozi wa kitaifa kuanzia aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, mawaziri, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na sasa Amos Makala. Ujenzi huo unatekelezwa na NHC na mshauri mwelekezi M/Scons Africa Limited na FB Consultant.

Septemba 16, 2019, hayati Magufuli aliyefikwa na mauti Machi 17 mwaka huu, alifanya ziara ya kushtukiza kukagua mradi huo, licha ya kuelezea kutoridhishwa na mazingira ya eneo, pia alisema wazi kuwa kasi ya ujenzi wa machinjio ya kisasa ilikuwa ndogo, hivyo kutoa ishara kuwa mradi usingekamilika kwa muda uliopangwa.

"Haiwezekani jengo la ghorofa moja lijengwe kwa miezi 18. Natoa maelekezo kuwa ndani ya miezi mitatu, yaani Oktoba hadi Desemba 31 mwaka huu (2019), ujenzi uwe umekamilika," aliagiza hayati Magufuli wakati huo.

Kutokana na agizo hilo, Makonda alivalia njuga utekelezaji wa mradi huo, huku Waziri Mkuu Kassim Majaliwa naye akifanya ziara eneo hilo kuhakikisha agizo la mkuu wa nchi linatekelezwa.

Hata hivyo, licha ya ziara za kushtukiza na maagizo kadhaa ya viongozi, mradi huo haujakamilika hadi sasa, lakini kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri utekelezaji umefikia asilimia 96, huku mkandarasi akiwa ameshalipwa zaidi ya Sh9 bilioni.

Kaimu Mkurugenzi Uendeshaji Biashara wa NHC, Margaret Ezekiel anasema miongoni mwa changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa mradi huo ni fedha kiasi cha uongozi wa shirika hilo kulazimika kutumia vyanzo vya ndani kuutekeleza.

Kutokana na taarifa za utekelezaji huo na uhakika kuwa suala la upatikanaji wa fedha limeshapatiwa ufumbuzi, ndipo Makala alipotoa amri kwa uongozi wa NHC kuhakikisha utekelezaji wa mradi huo unafanyika usiku na mchana kuwezesha kazi kukamilika ifikapo Agosti Mosi, mwaka huu.

Sisi *Mwananchi* tunaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huo ambao sio tu utaweka mazingira bora, safi na yenye kulinda afya za walaji wa kitoweo cha nyama, bali pia utabadilisha maisha na uchumi wa wakazi wa Dar es Salaam. Ni vyema changamoto zote zinazokwamisha utekelezaji wake zipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Wenye dhamana ya kutoa fedha wafanye hivyo kwa wakati na kwa kiwango sahihi, huku wanaotekeleza mradi nao wakitimiza wajibu wao kwa kasi na viwango.

Kwa hakika hakuna lugha nzuri ya kutumia kueleza suala la kusuasua kwa mradi huu, zaidi ya tabia ya baadhi ya watendaji katika ofisi za umma kutotimiza wajibu au kufanya kazi kwa mazoea. Haiwezekani mradi uliopaswa kukamilika Desemba, 2019 uwe haujakamilika hadi sasa Julai, 2021 licha ya ziara na maagizo mbalimbali kutoka kwa viongozi, akiwemo mkuu wa nchi.

Tunawasihi wanaohusika kuhakikisha mradi huu unakamilika na kuanza kutumika Agosti mosi kama alivyoagiza Makala, ambaye pia tunamshauri afuatilie kwa karibu utekelezaji wa agizo lake.

Scanned with CamScanner

HABARILEO JUMAPILI JULAI 11, 2021

# Dk Mwinyi aeleza manufaa utafiti sekta ya uvuvi, rasilimali za bahari

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema ujenzi wa jengo la Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Rasilimali za Baharini utafanikisha azma ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha kuzalisha mazao ya baharini yatakayoendana na uchumi wa buluu.

Alisema hayo wakati akizindua Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Rasilimali za Baharini, mkoa Mjini Magharibi juzi.

Akizungumza na wananchi na wadau wa sekta ya uvuvi, Dk Mwinyi alisema sekta hiyo ndiyo kiongozi katika uchumi mpya wa buluu na kwamba azma ya serikali ya kuwa na uchumi huo haiwezi kukamilika endapo hakutakuwa na utafiti, hivyo kukamilika kwa jengo hilo ni muhimu katika kufanikisha azma hiyo.



Alisema miongoni mwa kazi za taasisi hiyo ni kufanya utafiti wa rasilimali za bahari na kutoa vyeti vya ithibati vya ubora wa mazao ya baharini kwa wawekezaji watakaowekeza katika viwanda vya kusarifu samaki.

Dk Mwinyi pia alikagua ujenzi wa Soko Malindi na kuwaeleza wavuvi kuwa, serikali inakusudia kuhakikisha wanatumia vyombo vikubwa na vya kisasa vyenye uwezo wa kuwafikisha kwenye maji ya kina kirefu ili wapate tija ya kazi wanazofanya.

Alisema hatua hiyo itaondoa uwezekano wa vitendo vya uharibifu wa mazingira ikiwamo uvuvi haramu na kuitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wavuvi kukaa pamoja kubaini watu wanaoendesha vitendo hivyo.

Scanned with CamScanner

# Familia zahamasishwa ufugaji samaki

WATANZANIA wamehamasishwa kuchangamkia fursa ya ufugaji wa samaki katika ngazi ya familia na kibiashara kwa gharama inayoanzia Sh milioni 5.5 ili kujiongezea kipato na kupata kitoweo.

Hamasa hiyo ilitolewa na Meneja Mradi wa Ufugaji Samaki wa Suma Ponic unaosimamiwa na shirika la Suma JKT lililopo chni ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Kelvin Ngondo alipokuwa akizungumza na HabariLEO katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF).

Alisema Suma JKT ilianzisha mradi huo mwaka 2017 baada ya kubaini watu wengi Dar es Salaam wanatamani kufuga samaki kama wanavyofuga kuku, lakini kuna uhaba wa maeneo.

Alisema walitumia fursa hiyo kuanzisha mradi unaotumia eneo dogo na wenye matokeo makubwa.

Meja Ngondo alisema eneo la mita za mraba 100 linatosha kuanzisha mradi wa ufugaji samaki ngazi ya familia na kumpa mtu matokeo makubwa kuliko angefuga bwawani.

"Kun aina tatu za ufugaji samaki, ya kwanza ni wa familia unaotumia matangi yaliojengwa kwa saruji ya lita 5,000 za maji yenye uwezo wa kuchukua samaki kilogramu 120 hadi 130 ambao ni sawa na samaki 500 na gharama yake hadi kufungiwa ni Sh milioni 5.5."

"Ya pili ni ya kati iitwayo standard ya lita 10,000 inayogharimu Sh milioni 9.5 na inachukua samaki 1,000 na ya mwisho ni ya kibiashara zaidi, hii gharama yake ni Sh milioni 16 na inachukua samaki 1,500 mpaka 2,000 na lita za maji 30,000," alisema.

Kwa mujibu wa Jeja Ngondo, wameshawafungia mradi huo watu zaidi ya 24 tangu mradi uanze na wametoa mafunzo kwa zaidi ya watu 500.

Alisema mradi wa Suma JKT ndio wenye gharama nafuu zaidi kwa kuwa wamelenga kuwasaidia wananchi kufuga kitaalamu na kuwtaaka wafike katika banda lao la maonesho kupata elimu zaidi au baada ya maonesho kwenda Mbweni JKT kwenye mradi huo ili kujifunza zaidi.

"Mfugaji hupewa vifaranga vyenye miezi miwili kulingana na aina ya ufugaji anaotaka na baada ya miezi minne huvuna samaki. Mtaani kilo moja ya samaki huuzwa kwa zaidi ya Sh 10,000," alisema.

Alisema waliamua kushirikisha zaidi wananchi katika mradi huo kutokana na miaka ya nyuma kutokea udanganyifu mwingi katika ufugaji wa samaki na kufanya watu wakate tamaa.

Habari Leo Uk.5, Julai 11,2021

Scanned with CamScanner

TAFAKURI    UHURU UK 6    Julai 11, 2021

# *Wanawake tumieni fursa ya ufugaji, uvuvi kujiinua kiuchumi



Na IRENE MWASOMOLA
0654415116
irenemwasomola@gmail.com

MWANAMKE ni jeshi kubwa hii ni kauli inayoakisi uhalisia wa uwezo wa mwanamke katika mapambano ya kujikwamua kiuchumi.

Ufugaji na uvuvi ni sekta muhimu ambazo wengi huamini kuwa wanaume ndiyo wanaostahili kujishughulisha nazo, dhana ambayo ni potofu katika maisha.

Imeshuhudiwa mara kadha wanawake wakijikita katika shughuli ndogondogo ndani ya sekta hizo, kama uvuvi wengi wao huishia kupokea samaki kutoka katika mashua bada ya kuvuliwa na wanaume.

Wengi hufanya hivi wakiamini hawana uwezo zaidi ya wanachokifanya, huku wakigubikwa na mitazamo kuwa uvuvi wa kuingia baharini au ziwani ni stahili ya wanaume pekee.

Shughuli ndogondogo hizo wanazofanya huwaingiza kipato kidogo kisichotosheleza hata mahitaji ya familia, hivyo wanajikuta wakiwajibika muda mwingi usiolingana na fedha wanazoingiza.

Ni ukweli usiopingika kuwa wapo wanawake lukuki waliofanya mageuzi makubwa katika shughuli mbalimbali, lakini wamesahau sekta ya mifugo na uvuvi zenye fursa kubwa katika kujikwamua.

Ni imani yangu kuwa, hatua ya serikali kupanga mkakati wa kuziboresha sekta hizo, itawapa chachu wanawake kuzichangamkia kutokana na fursa nyingi zilizopo ndani yake.

Itakumbukwa serikali katika mwaka huu wa fedha, imeahidi kununua meli nane kubwa za uvuvi na maboresho mengine katika sekta ya mifugo ikiwemo matumizi ya teknolojia katika malisho, hatua ambazo zinatarajiwa kuwanufaisha wadau wa sekta husika.

Pamoja na mambo mengine, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, aliwahi kubainisha kuwa serikali imefuta tozo baadhi ya kodi zilizokuwa zinakwamisha maendeleo ya sekta ya mifugoi nchini.

Pia, ili kuboresha sekta hiyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Bank ya Kilimo (TaDB) itatoa mikopo kwa vikundi vya wafugaji ambapo sh. bilioni 20 zimetengwa kufanikisha hilo.

> Itakumbukwa serikali katika mwaka huu wa fedha, imeahidi kununua meli nane kubwa za uvuvi na maboresho mengine katika sekta ya mifugo ikiwemo matumizi ya teknolojia katika malisho, hatua ambazo zinatarajiwa **kuwanufaisha wadau wa sekta husika**

Bila shaka, mageuzi haya yatafuta mtazamo kuwa wanaume ndiyo wanaopaswa kuwa wavuvi na wafugaji pekee, badala yake hata wanawake watajikita katika shughuli hizo ili kuwa sehemu ya wanufaika wa fursa zilizozalishwa kwa juhudi za serikali.

Aidha ni wajibu wa wanawake kuchangamkia fursa hizo kwa kuchapa kazi kwa bidii ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, kukuza uchumi wa taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Kwani sekta hizo ni daraja tosha la kuwakomboa vijana na wanawake wote sio wa vijiini pekee bali hata na mjini.

Pia ni wakati wa wanawake kujihusisha na ufugaji wa kisasa ili kuzalisha bidhaa zitakazokidhi soko la kimataifa.

Kutokana na mafanikio haya nawiwa kuipongeza serikali chini ya Rais Samia kwa namna alivyoboresha na kusimamia sekta ya mifugo na uvuvi ili kuwanufaisha wadau.

Habari Leo Uk.15, Julai 11,2021

# Wakulima wa mwani Mtwara walalamikia bei

**Na Sijawa Omary, Mtwara**

WAKULIMA wa zao la Mwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara wamelalamikia uwepo wa bei ndogo kwenye zao hilo ikilinganishwa na ugumu wa kilimo hicho.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na wakulima wa zao hilo la Mwani wakati wa mafunzo ya siku moja yaliyofanyika Mjini Mtwara ya kuwajengea uwezo zaidi namna ambavyo wanaweza kuboresha kilimo hicho na kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Mafunzo yameshirikisha wakulima kutoka vijiji vya Naumbu pamoja na Mkungu chini ya Kampuni inayojihusisha na masuala ya kusafirisha mizingo Duniani (DHL) na Shirika lisilo la Kiserikali linalojihusisha na masuala mbalimbali ya kijamii mkoani Mtwara la MSOAPO.

Mkulima kutoka Kijiji cha Mkungu Kikundi cha Juhudi kwenye halmashauri hiyo, Sharifa Abdallah alisema wamekuwa na jitihada kubwa ya kulima kilimo hicho lakini bei ni ndogo, hivyo ombi lao kwa serikali kuliangalia zao la Mwani liweze kupata soko la uhakika.

Asia Selemani kutoka Kijiji cha Mkungu kwenye Kikundi cha Jitegemee alisema kuwa kwa sasa kilo moja ya zao hilo wanauza Sh 500 ambayo ni ndogo.

Mratibu wa Shirika la Msoapo, Mustafa Kwiyunga alisema mafunzo hayo yamekuja baada ya kuona vikundi na wakulima hao bado hawana uwezo wa kujiendesha wenyewe.

Scanned with CamScanner

Habari Leo uk.5
Julai 11,2021

# Narco kuingiza soseji za viwango Septemba

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ranchi za Taifa (Narco) inatarajia kuzindua soseji wanazotengeneza wenyewe ikiwa ni hatua ya kuhakikisha wanalinda afya za wananchi kwa kula bidhaa yenye uhakika wa viwango na pia kuchangia katika uchumi wa nchi.

Akizungumza na HabariLEO katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), Ofisa Masoko na Mahusiano wa Narco, Jumanne Mutalemwa, alisema bidhaa hiyo 'Kongwa Beef Sausage' itaingia sokoni Septemba mwaka huu na itatoa fursa kwa watu hasa vijana kuwa wakala wa kuuza ili kujipatia ajira na kipato.

"Bidhaa hii ni yetu Watanzania, tulizoea kwa muda mrefu kutumia sausage (soseji) kutoka nje ya nchi ambazo hatuna uhakika na ubora wa nyama wanazotengenezea, hii inatengenezwa katika ranchi yetu ya Kongwa kwa kutumia nyama ya ng'ombe wetu wa asili, ni salama kwa watu na tuna uhakika nayo asilimia zote," alisema.

Alisema Septemba bidhaa hiyo itaanza kuingizwa sokoni kupitia maduka yao yaliyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Bukoba na Kongwa kwenyewe na katika ranchi zote zilizo chini ya Narco.


Mutalemwa alisema pia kuwa bei zitatangazwa baadae kwa kuwa sasa mtambo wa kuanza kutengeneza ndio unafungwa. Hata hivyo aliwataka vijana wanaopenda kujiajiri, wajiandae kutumia fursa ya kuwa wakala wa Narco kwa kuchukua bidhaa hiyo katika maduka yao kwa bei ya jumla na kuuza.

"Moja ya kazi kubwa ya serikali ni pamoja na kuhakikisha usalama wa chakula kwa afya ya watu wake. Kama mnavyofahamu Narco inasimamia ubora wa nyama siku zote hivyo watasambaza bidhaa hiyo wenyewe lakini pia watatumia wakala kwa utaratibu maalumu watakaouweka ili kulinda afya ya walaji," alisema.

Scanned with CamScanner

# Waziri Ndaki afunguka mafanikio Wizara ya Mifugo na Uvuvi siku 100 za Samia

NA MWANDISHI WETU



SIKU 100 tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarani zimekuwa za mafanikio makubwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwani katika kipindi hicho imetekeleza kazi mbalimbali.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki anasemaa kazi hizo ni zile zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, Waziri Ndaki anasema baadhi ya kazi hizo zimetokana na maelekezo ya Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika matukio mbalimbali ili kuboresha Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Hivyo haya ni baadhi ya mafanikio ambayo yamepatikana katika siku 100 za utawala wa Rais Samia kama yanavyoelezwa na Waziri Ndaki.

TEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

Waziri Ndaki anasema katika kipindi cha siku 100 ya Serikali ya Awamu ya Sita, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mifugo ni pamoja na ujenzi wa visima virefu viwili (2) katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Usolanga) na Mpapa (Manyoni) vimefikia asilimia 70 na asilimia 30 mtawalia. Pia, ukarabati wa mabwawa matatu (3) ya Chamakweza (Chalinze), Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro) umekamilika kwa asilimia 100.

Anaeleza mafanikio mengine ni kwamba jumla ya hekta 32,044.21 zimetengwa katika Wilaya za Tanganyika, Nsimbo na Mlele kwa ajili ya malisho.

Vile vile Waziri Ndake anafafanua zaidi katika kipindi hiki Serikali imetoa mafunzo na leseni kwa wachunaji ngozi 340 wa machinjio za Manispaa ya Kinondoni na Temeke Dar es Salaam.

Pia, imewapatia vitendea kazi Wakaguzi wa Ngozi 34 wa Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara. Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya viwanda.

"Mnada wa mifugo wa mpakani wa Magena, Mara umefunguliwa ili kuwezesha biashara ya mifugo kati ya Tanzania na Kenya. Pia, ujenzi wa mnada wa mifugo wa upili wa Buzirayombo, Geita umefikia asilimia 50. Lengo ni kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi," anasema Waziri Ndaki na kuongeza,

"Jumla ya ng'ombe wa asili 146 katika mkoa wa Iringa na ng'ombe 152 katika mkoa wa Singida walifanyiwa uchambuzi ili kubaini na kutunza mbari za ng'ombe wa asili,".

Kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zimefanya kikao na kukubaliana kuendeleza ushirikiano kiutendaji katika ngazi za idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo.

"Lengo ni kuimarisha sekta za mifugo katika pande mbili za muungano ili ziweze kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi,".

TEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI

Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi Waziri Ndaki anasema ni moja kati ya sekta za kiuchumi hapa nchini.

Anasema shughuli za uvuvi huchangia katika kuwapatia wananchi uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato, kupunguza umaskini, kupata fedha za kigeni na kuchangia kwenye pato la Taifa.

Anataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 za uongozi wa Awamu ya Sita kuwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Majengo Matatu ya Ofisi za Vikundi vya usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMU) katika Wilaya za Pangani (Kipumbwi), Mkinga (Zingibari) na Bagamoyo (Dunda).

Anafafanua kwamba ni katika kipindi hiki ambapo kumekuwa na juhudi za maboresho ya miundombinu wezeshaji ya shughuli za uvuvi kwa kuanza ujenzi wa mialo sita (6) katika Kanda ya Ziwa Victoria, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay-Nyasa Mkoani Ruvuma, na kutangazwa kwa zabuni ya kupata Mkandarasi wa Ukarabati wa Soko la Samaki la Feri-Dar es Salaam utakaoanza mwezi Julai 2021.

Vile vile anataja mafanikio mengine kuwa ni kutengwa kwa fedha za ndani shilingi bilioni 50 katika bajeti ya 2021/2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Mbegani Bagamoyo.

Waziri Ndaki anaendelea kusema kuwa Wizara imefanikisha kuzinduliwa kwa Dawati la Jinsia katika Sekta ya Uvuvi ili kuwawezesha wanawake kushiriki ipasavyo katika uchumi wa buluu kupitia Sekta ya Uvuvi pamoja na kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 ya tarehe 23 Aprili, 2021.

Lakini pia imetangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya uvuvi kupitia mikutano ya kitaifa iliyojumuisha wageni kutoka Ufalme wa Saudi Arabia, Jamhuri wa Watu wa China, na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Aidha, hii ilifanikisha Juni 22, 2021 kwa mara ya kwanza Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kukusanya jumla ya Dola za Marekani 800, 000 sawa na TSH 1.84 bilioni malipo ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu kwa meli 22 baada ya meli za kigeni kusitisha kuchukua leseni za Tanzania mwaka 2017/2018 kulikosababisha Serikali kukosa mapato na DSFA kushindwa kujiendesha yenyewe.

Aidha anasema ni katika kipindi hiki Wizara imefanikisha ununuzi wa maboti kumi na mbili (12) na injini sita (6) za kupachika kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi ambapo pia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) imefanikiwa kuwawezesha wavuvi 100 katika ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kuvua kwa ufanisi kwa kuwapatia taarifa za maeneo yenye samaki Baharini.

Waziri Ndaki anaeleza kwamba katika kipindi hiki DSFA pia ilikamilisha maandalizi na kuwezesha Mawaziri wenye dhamana ya Sekta ya Uvuvi SMT na SMZ kusaini Kanuni Mpya za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2021 na kuanza kutumika rasmi tarehe 23 Aprili, 2021.

Vile vile DSFA imeimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi na shughuli haramu zinazohusiana na uvuvi katika eneo la ukanda wa uchumi wa bahari (EEZ) inalolisimamia kwa kutumia mifumo yake ya kufuatilia mienendo ya meli ambapo ambapo tarehe 23 Aprili, 2021 ilinasa na kufanikisha kukamatwa kwa mashua Hg iliyokuwa ikipeperusha bendera ya Iran iliyokuwa na kilogramu 859.36 za madawa ya kulevya.

Anasema kwamba ili kunufaika na fursa za Uchumi wa Buluu kupitia tasnia ya ukuzaji viumbe maji, Serikali imetenga shilingi bilioni 18 ambazo zitatumika kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu katika vituo sita (6) vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Mwamapuli–Tabora, Ruhila– Ruvuma, Kingolwira–Morogoro, Nyengedi – Lindi, Machui–Tanga, na Rubambagwe–Geita.

Anaeleza hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa vifaranga bora vya samaki kwa kuongeza uzalishaji kutoka vifaranga milioni 2 hadi kufikia milioni 8 kwa mwaka na kuboresha utoaji wa huduma za ugani hususani kutoa mafunzo kwa vitendo kwa angalau wananchi 3,000 ili kuhamasisha na kuwezesha ufugaji samaki na viumbe maji wengine kwa tija na faida na kupanua wigo wa huduma za ugani.

Lakini pia itasaidia kuanzisha mashamba darasa 40 ya ufugaji samaki yatayosimamiwa na vikundi vya vijana na kinamama.

Kwamba huu ni mwanzo wa utelekezaji wa azma ya kuwa shamba darasa katika kila halmashauri nchini ili kuhamasisha ufugaji wa samaki nchini kwa ajili ya kuboresha lishe, kuongeza kipato na kukuza uchumi.

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.5, Julai 11,2021

HABARI KITAIFA

# Wizara yalipa jeshi vifaranga vya samaki

Na Renatha Msungu

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imetoa vifaranga vya samaki 25,000 kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kuongeza uzalishaji wa samaki katika mabwawa ya Kikosi cha 837 Chita KJ kilichoko mkoani Morogoro.

Kikosi hicho kinafanya miradi ya ufugaji samaki na kilimo cha mpunga.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ziara ya kukagua miradi ya kimkakati inayofanywa na JKT katika kikosi hicho, Mkurugenzi wa ukuzaji viumbe maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Nazael Madala, alisema wizara imefanya hivyo baada ya kuona juhudi zinazofanywa na JKT katika ufugaji wa kisasa.

Alisema vifaranga hivyo ambavyo ni wazazi, vinakwenda kuongeza nguvu

katika uzalishaji wa samaki aina ya sato unaofanywa na kikosi hicho.

"Hivi sasa JKT watakuwa na uwezo wa kutotolesha vifaranga 500,000 na kupelekea kufikia kuzalisha samaki milioni sita, jambo ambalo litaongeza uzalishaji katika taifa," alisema Madala.

Alisema kitotoleshi cha samaki cha JKT kitafanya idadi ya vitotoleshi nchini kufikia 34 na hiyo inafanya uzalishaji wa samaki nchini kuongezeka kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali.

Alitoa wito kwa wananchi kuhamasika kufuga samaki kwa kuwa ni fursa ya kuongeza lishe na kipato.

Mkurugenzi Madala alisema kikwazo katika ukuaji wa samaki nchini ni ukosefu wa vifaranga, ndiyo maana wametoa vifaranga hivyo ambavyo ni wazazi kwa JKT ili viende kusaidia uzalishaji wa samaki aina ya sato na kupunguza uhaba wa vifaranga vya samaki.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema JKT iko mstari wa mbele kuhakikisha miradi ya kilimo na mifugo inasonga mbele katika vikosi mbalimbali vya jeshi hilo.

Kanali Mabena alisema kuwa baada ya serikali kutoa agizo kwa majeshi yasaidie kujitegemea katika vyakula, ndipo JKT walibuni kilimo mkakati ambacho hivi sasa kinawasaidia kuzalisha mazao ya chakula na biashara.

Alisema hivi sasa wanakwenda kuzalisha mbegu bora ya zao la mpunga ambazo anaamini zitaisaidia jamii katika kuendesha kilimo bora cha mpunga.

"JKT tumejipanga kuhakikisha tunasonga mbele katika kilimo, tumeanza na ekari 12,000 lakini lengo letu ni kulima ekari nyingi ili kuhakikisha tunajitosheleza kwa chakula lakini pia chakula cha ziada kinauzwa nje ya jeshi," alisema.

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.2 , Julai 11,2021



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (katikati), akizungumza na mfugaji anayemiliki kitalu namba mbili, Primus Karokola (kulia), wakati alipotembelea kuangalia mifugo iliyopo kwenye ranchi ya Mabale, wilayani Misenyi, mkoani Kagera jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wizara hiyo, Prof. Elisante Ole Gabriel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Scanned with CamScanner